

## HALMASHAURI YA MJI KIBAHA



### TAARIFA KWA UMMA

SHILINGI 249,240,000/- KUSAIDIA VIKUNDI 76 MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE, VIJANA NA WENYE ULEMAVU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

*Kibaha, Jumatano 17 Februari, 2021*

Mkurugenzi wa halmashauri ya Mji Kibaha Jenifa Omolo ameendelea kutekeleza agizo la serikali la kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu kama sehemu ya mtaji katika miradi waliyoibuni, kuiandikia maandiko na kuyawasilisha ofisi ya Mkurugenzi.

Katika kipindi hiki, halmashauri imepokea maombi ya vikundi sabini na sita (76) vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vilivyopitishwa katika kata 14 zinazounda halmashauri ya mji Kibaha yenye thamani ya shilingi 464,099,700/-

Aidha, Halmashauri kupitia wataalam wa idara ya maendeleo ya jamii kuanzia ngazi ya Mtaa, Kata kwa kushirikiana na waliopo ofisi ya Mkurugenzi wamejadili na kuchambua maombi hayo kwa mchanganua ufuatao; Vikundi 53 vya wanawake vyenye thamani ya shilingi 141,950,000/- Vikundi 21 vya vijana vyenye thamani ya shilingi 99,550,000/- na vikundi 2 vya watu wenye ulemavu vyenye thamani ya shilingi 7,740,000/- vimekidhi vigezo vya kupata mkopo huo baada ya majadiliano, maridhiano na maelekezo ya wataalam wa idara ya maendeleo ya jamii wanaoratibu zoezi hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Mussa Ndomba ametoa rai kwa wanufaikaji wote kwenda kutumia fedha walizokopeshwa kwenye malengo waliyokusudia ili kujiongezea kipato. Aidha, amewakumbusha kuwa wasichukulie fedha hizo kama zawadi kwani wanapaswa kuzirejesha ili wengine wakopeshwe.

Ndomba amewaahidi Watanzania hususan wanakibaha kuwa, Halmashauri itaendelea kutekeleza agizo hilo la serikali kadri inavyokusanya mapato yake ya ndani huku akitoa ngalizo kwa waratibu kutenda haki kwa vikundi vyote vinavyoomba na kukidhi masharti ya mkopo

***“Kibaha yetu, Maendeleo yetu, Kwa pamoja tunaweza”***

Imetolewa na;

Innocent Byarugaba  
OFISA YA MAWASILIANO, HABARI NA UHUSIANO  
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA